

NAMNA YA KUJIFUNZA MUZIKI TANGU KUZALIWA KWA MTOTO:

- Mpatie mtoto nyimbo na ala za sauti au michezo ya ala za sauti ambayo inachochea kinachopendelewa na ushiriki/uguswaji wa hisia.
- Cheza michezo ya ala za sauti na nyimbo pamoja na mtoto ambayo inamfaa mtoto.
- Wezesha ala za sauti za kimuziki na kimawasiliano kwa mtoto yakiwa na hisia chanya na kuwepo pamoja.

MAWASILIANO YA ALA ZA SAUTI:

- Kama mtoto anaonesha ala ya sauti, Unaweza ukamwitikia mtoto kwa ala ya sauti ile ile (mfano, kupitia sauti au kumgusa kwa mapigo ya sauti yaliyo sawa).
- Kwa njia hii, unaweza kupata hadi majibizano ya hisia yasiyo ya kuongea na mtoto.
- Kila mara msaidie mtoto kwa upole katika majaribio ya kuwasiliana kwa ala za sauti au mapigo ya sauti.
- Unaweza kutumia ala za sauti kurekebisha hisia za mtoto (mfano, kumbembeleza mtoto kimapigo ya sauti taratibu na kwa upole pale anapolia).



NYIMBO:

- Unapoimba wimbo kwa mtoto, kuwa makini na hisia za mtoto.
- Mtoto anapolia, au anapoenda kulala, imba wimbo kwa sauti laini ya chini taratibu.
- Mtoto anapokuwa na furaha au anataka kucheza, imba kwa sauti ya juu wimbo wa haraka unaosikika.

MICHEZO KATIKA UKUAJI WA MTOTO:

Mpatie mtoto michezo inayowezesha:

- Mawasiliano/matamshi ya ukuaji wa **lugha**, mfano, Kuimba nyimbo kwa pamoja.
- Ukuaji wa **akili**, mfano, kucheza na vibao vyenye namba.
- Ukuaji wa **viungo**, mfano, kupiga makofi.
- Ukuaji wa **hisia**, mfano, kuendeleza kucheza kutokana na desturi au uzoefu.
- Ukuaji wa **kijamii**, mfano, kucheza pamoja na watoto wengine.

Itikia kwa upole kwa:

- Majaribio ya mtoto kuongea wakati wa mchezo.
- Majaribio ya mtoto kutatua matatizo yao wakati wa mchezo.
- Majaribio ya mtoto kusogea wakati wa mchezo.
- Kujieleza kwa hisia kwa mtoto wakati wa mchezo.
- Majaribio ya mtoto kwenda kukutana na wengine wakati wa mchezo.



AINA ZA MICHEZO:

- Wajengee watoto hali ya kujizoeshwa aina mbalimbali za michezo kutokana na hatua ya ukuaji wa michezo.
- Zingatia kwamba kila mtoto ni tofauti katika ukuaji na watoto wanaweza kuchelewa katika ukuaji wa michezo yao.





HATUA ZA UKUAJI WA MCHEZO:

- Mpe mtoto mchezo wa mtu na mtu, mfano, mchezo wa kuficha na kuonesha sura.
- Mpe mtoto mchezo wa mtu na mtu kwa kutumia vitu.
- Mjengee mtoto mazingira ambayo yatamuwezesha kucheza mwenyewe.
- Mjengee mtoto mazingira ambayo yatamuwezesha kuwaangalia watoto wengine.
- Mjengee mtoto mazingira yatakayomuwezesha kucheza sambamba na watoto wengine.
- Mjengee mtoto mazingira yatakayomuwezesha kuiga wengine.
- Mjengee mtoto mazingira yatakayomuwezesha kucheza na wengine.

Msaidie mtoto katika:

- kujaribu kugundua vitu na mazingira yaliyo nje na aliyoyazoea.
- hitaji la kucheza mwenyewe.
- hitaji la kuangalia uhalisia.
- Hitaji la kucheza sambamba.
- Kuiga.
- Majaribio ya ushirikiano.



MAELEZO KWA AJILI YA MAWASILIANO

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:

**KITUO CHA WATOTO YATIMA IRENTE
SIMU:**

**0754 844 777
0714 157 837**

MHUSIKA:



IRENTE CHILDREN'S HOME

© 2019 Prof. Dr. Ulrike Lütke,
Leibniz Universität Hannover
– All Rights Reserved –

ulrike.luedtke@ifs.uni-hannover.de



Niedersächsisches Ministerium
für Soziales, Gesundheit
und Gleichstellung

Kipeperushi hiki kimetengenezwa kwa msaada wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Afya na Fursa Sawa ya Jimbo la Lower Saxony, Ujerumani

MAFUNZO YA MALEZI YA AWALI NA MAKUZI YA MATAMSHI NA LUGHA KITUO CHA WATOTO YATIMA IRENTE, FEB 2018 - SEP 2019



MICHEZO NA MUZIKI

Tunawashukuru washiriki wote wa Mafunzo kwa kutunga maudhui na kupigapicha mbalimbali zilizomo kwenye kipeperushi hiki.

Kwa sababu za kimaadili, tunadiriki kutoonyesha sura za watoto walioko kwenye picha.